JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS -TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE

SHULE YA SEKONDARI ILUMAKI,
S.L.P. 2 6,
MAKETE.

20/12/2020.

SIMU NA:-
MKUU WA SHULE; 0762 – 513876
MAKAMU MKUU WA SHULE; 0765316900

Kumb. Na. ILU/SS/02/2020/11

Jina la Mwanafunzi ……..

Namba ya Mtihani ……
Shule ya Msingi ILEVELO/LUPALILO/UGABWA/MAGO/KISINGA

MAKETE.

MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI ILUMAKI

1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba Umechaguliwa kujiunga na masomo ya Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari ILUMAKI mwaka 2021. Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2020 Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 08/01/2021 ukiwa umeongozana na mzazi/mlezi wako.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 Sare ya Shule

a) **WAVULANA ;**

Sare ya Shule hii ni Suruali mbili, rangi ya kahawia 1 rangi bluu bahari 1, Mashati mawili meupe ya mikono mifupi, sweta 2 za kijani Jeshi (zenye mshono wa .V. Shingoni), viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba jozi mbili visivyo na kisigino kirefu, soksi nyeusi jozi 3 na T-shirt 1 Shilingi 10,000/= inapatikana Shuleni.

Mavazi mengine kwa wavulana ni ; track suit nyeusi zenye mikanda mitatu mweupe iliyonyooka jozi mbili (2), koti jeusi lisilo na maandishi 1 na Raba kwaajili ya michezo.

N.B: Nguo zingine hazitaruhusiwa kabisa kuvaliwa Mwanafunzi awapo Shuleni.

b) **WASICHANA,**

Suruali mbili , rangi ya kahawia 1 na rangi ya bluu bahari 1 (zisizobana), sketi mbili rangi ya kahawia 1 na rangi ya bluu bahari za rinda kati ya 8-12 (sketi itavaliwa kwa wakati mmoja na suruali) Shati mbili nyeupe za mikono mifupi tetron – Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba jozi mbili visivyo na kisigino kirefu, sweta mbili rangi ya kijani jeshi (zenye mshono wa .V. Shingoni), soksi nyeusi jozi 3, T-shirt Shilingi 10,000/= inapatikana shuleni.

Mavazi mengine kwa wasichana ni ; track suit nyeusi jozi mbili, koti jeusi lisilo na maandishi, Raba kwaajili ya michezo, Gauni 2 (Shamba dress 2) damu ya mzee 1 na bluu bahari 1, kanga jozi moja (1), pedi, under were za kutosha (nguo za ndani) na Hijabu – rangi Nyeupe(kwa Waislamu)

N.B: Nguo zingine hazitaruhusiwa kabisa kuvaliwa Mwanafunzi awapo Shuleni.

c) **Mahitaji ya hosteli kwa wavulana na wasichana ;**

Wanafunzi watatakiwa kuja na godoro futi 2.5 (futi mbili na nusu), Mashuka mawili rangi ya pinki 1 na light bluu 1, Tranka kwa ajili ya kutunzia vitu vyake, blanketi nzito, taulo, ndoo ndogo 2, bakuli (Kontena), kijiko, kikombe, dawa ya mswaki, mswaki, kiwi ya viatu na ndala za kuogea.

d) **Mahitaji ya taaluma kwa wanafunzi wote ;**

1. Daftari kumi (10) Count book,
2. Kalamu wino na Penseli za kutosha
3. Mkebe wa hesabu (Mathematical set.
4. Kamusi 1 ya English-kiswahili)
5. Vitabu vya kujisomea (Mabala the Farmer/ Hawa the Bus Driver)

e) **Mahitaji ya Kamati ya Chakula na Malazi**

2.2 Mchango wa Chakula 360,000/= kwa mwaka. Inalipwa kwa awamu 2, awamu ya kwanza 180,000/= awamu ya pili 180,000/=

2.3 Mchango wa kitanda 50,000/=

2.4 Bunda moja la karatasi **A-4**

2.5 Mopa 1 na Brashi 1 Kwaajili ya usafi wa Hosteli

2.6 Jembe lenye Mpini 1

2.7 Kwanja 1

3.0 Sheria na Kanuni Muhimu za Shule hii

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya Mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima ;
b) Mahudhuria mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima ;
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation) ;
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa ;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii ;
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule ;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa ;
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote ; na
i) Kutunza mali za umma.

3.1 Makosa yafuatayo yaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa Shule

a) Kupigana au kupiga
b) Wizi
c) Ubakaji
d) Uasherati na ushoga
e) Kuoa au kuolewa
f) Kuwa na simu ya mkononi.
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kukataa adhabu kwa makusudi.
j) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
k) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
l) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

4.0 Mambo Mengine Muhimu yanayopswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

NB ;Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

CHRISTOMS BASIL MTURO
MKUU WA SHULE

Sehemu ya Mzazi/Mlezi.

Kwa Mzazi/Mlezi wa …….

1. Napenda kukupongeza kwa mwanao kuchaguliwa kujiunga **Kidato cha Kwanza** hapa ILUMAKI. Ni mategemeo ya Shule kuwa utajitahidi kwa uwezo wako wote kumsaidia ili aweze kusoma bila matatizo (kwa kumtimizia mahitaji yote ya muhimu).
2. Ili mtoto wako aweze kufanikiwa ni muhimu awepo shuleni muda wote wa masomo. Hivyo huna budi kumsaidia ili vikwazo visivyo vya lazima visiwepo.
3. Tafadhali jaza fomu iliyoambatanishwa kama inavyojieleza.

A: AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi ……..……. Mzazi/Mlezi wa ……..…… (jina la mtoto) ninakubali aingie Shule ya Sekondari ILUMAKI na ninaahidi kumtimizia mahitaji yote yaliyoagizwa. Pia naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule kumlea na kumtunza ki–Tanzania (awapo Shuleni na likizoni) mpaka atakapo maliza masomo yake.

Na kama kuna mabadiliko nitautarifu uongozi wa shule.

Anuani yangu ya kudumu: …….

…….

Sahihi. …… Tarehe ……

B: AHADI YA MWANAFUNZI.

Mimi …….. Nakubali/Sikubali* Nafasi niliyopewa katika Shule ya Sekondari ya ILUMAKI.

Naahidi kuwa nitazitii Sheria zote za Shule na kufuata maelezo na maagizo nitakayopewa na Mkuu wa Shule, Wafanyakazi wote na Viongozi wote wa Serikali ya Wanafunzi.

Nitashirikiana na wanafunzi wenzangu katika shughuli za masomo, elimu ya kujitegemea, michezo na kutunza usafi wa mazingira ya shule kwa muda wote nitakao kuwa ILUMAKI.

Shule niliyo soma ni …… Namba ya mtihani ni ……

Sahihi ……... Tarehe ……...

*Futa lisilohusika.

C: SEHEMU YA MGANGA (MEDICAL EXAMINATION FORM) .

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

MAKETE DISTRICT COUNCIL
ILUMAKI SECONDARY SCHOOL

This form must be completed by a Government Medical Officer

Name of Student.....
Age..... Sex.....

The above named pupil has been examined in respect of

a) PREGNANCY TEST (FOR GIRLS ONLY) .....
b) STOOL .....
c) URINE .....
d) CHEST .....
e) BLOOD .....
f) EYES .....
g) EARS .....
h) OTHER FINDINGS .....
.....
.....

I am satisfied that the above named pupil is fit/not fit for pursuing Secondary studies at ILUMAKI

..... **.....**
SIGNATURE **DATE**

..... **.....**
DESIGNATION and OFFICIAL STAMP **STATION**